

Mwaliko kwa wazazi

# Maelezo- na mkutano wa mazungumzo kuhusu kushirikisha majengo ya shule za chekechea na shule

**Manispaa ya Värmdö inawaalika kwenye mkutano wa maelezo na mazungumzo kuhusu kushirikisha majengo ya shule za chekechea /shule. Mkutano utakuwa wa kidigitali na utafanyika 29 septemba saa 18:00.**

Chanzo cha kushirikisha majengo ni kwamba maeneo mengi ya manispa ya shule na shule za chekechea yanakaa bure, yanahitaji utumiaji bora kwani majengo mengi yanayotumika si bora kwa watoto.

Ofisi ya elimu ina zoezi kukusanya baadhi ya shule na shule za chekechea za manispaa.

## Majengo sahihi na yenye ubora wa hali ya juu

Lengo ni kuongezea uwezokano wa kupata majengo sahihi yanayo changia kujenga shule na shule za chekechea za kudumu kipedagogia na kwa kiuchumi katika Värmdö. Mabadiriko yataleta kwa baadaye matumaini bora na kuendeleza vitengo vilivyobaki kuwa na huduma na ubora wa hali ya juu, na vile vile kujenga msingi mzuri kwa wanafunzi na maendeleo ya watoto wetu.

Pendekezo litafikishwa mpaka kwenye uamzi wa bodi ya elimu oktoba, kwa bodi ya manispa 28 oktoba, kwa diwani wa manispa desemba. Madiriko yatapitishwa pamoja na shule kufunguliwa agosti 2021.

## Shule na Shule za chekechea zinazohusika

Pendekezo linahusu shule za chekechea Kotten, Minimunkis, Lokatten, Blåsippan, Blomkulan, Åkerlyckan na Farstaborg. Kati ya hizo Åkerlyckan na Blomkulan zitachunguzwa na kuendelezwa majengo yaliopo na kazi zake. Kotten yote itahamishiwa kwenye shule ya chekechea Fågelviks. Watoto wa Minimunkis watakaribishwa kuhamia shule ya chekechea Munkmora, watoto wa Lokatterns kukaribishwa nafasi kwa shule ya chekechea Haghulta. Shule ya chekechea ya Farstaborg ilikuwa inasubiri kwa muda Shule ya chekechea ya Charlottendal ambayo itaisha mwanzoni wa 2021.

Shule ya Munkmora inapendekezwa kufungwa pamoja na kazi zake na kutokea Ekedal kuhamia Kvarnberget. Ili kuwezesha hivi darasa la mwaka wa nne litahamia kutokea Ekedal kwenda Kvarnberget. Kutokana na kazi muhimu za kijamii shule ya majengo ya Munkmoras itachunguzwa.

Mabadiriko ya Blåsippan yatafanyinka 2022.

## Maelezo- na mkutano wa maongezi 29 septemba

Värmdö kommun inawakaribisha wazazi wanaohusika kwenye mkutano wa kidigitali wa maelezo na maongezi 29 septemba saa 18 kwani pendekezo litaelezewa. Baada ya hapo kutakuwa na uwezo wa kuuliza maswali na kwa njia ya kuchati. Linki kwenda mkutano huu utatumwa pekee.

Watakaohudhuria kutoka Värmdö kommun ni Peter Bergström, meneja wa elimu, Cecilia Lindberg, mwenyekiti bodi wa elimu, Fredrik Sneibjerg, makamu wa bodi wa elimu, Ingmarie Lagne, meneja wa shule ya msingi, Mats Lundström, meneja wa shule na msimamizi Erik Sanner, meneja wa kitengo uendeshaji na ubora.